



ATHARI YA MADINI YA RISASI KWA WATOTO

Watoto wanaweza Kuathiriwa na Risasi kwa Urahisi Kabisa

Je, Mtoto wangu Anaweza Kuathiriwa na Madini ya Risasi?

Njia pekee ya kujua iwapo mtoto wako ameathiriwa na madini ya risasi ni kupima damu yake. Inapendekezwa kwamba watoto wapimwe wakiwa na umri wa mwaka mmoja na miwili. Mpeleke mtoto wako akapimwe ikiwa amekuwa katika hatari hizi:

- Kuishi au kutembelea nyumba iliyojengwa kabla ya 1978 yenye hatari za madini ya risasi au inayokarabatiwa
- Kuhudhuria kituo cha kutunzia watoto kilichojengwa kabla ya 1978 penye hatari za madini ya risasi au inapokarabatiwa
- Kushinda na ndugu, jamaa, au mchezaji mwenzake ambaye ameathiriwa na madini ya risasi
- Kushinda na mtu anayetumia madini ya risasi kazini au kwingine (k.m. uvuvi, kupaka rangi, kutengeneza gari)
- Kula chakula kilichowekwa kwenye chungu kinachong'aa au chombo kilichoumbwa kwa madini ya risasi
- Kutumia tiba asili na bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi (k.m. Kohl, Azarcon, Alarcon, Greta, Pay-loo-ah)

DALILI ZA KUATHIRIWA NA RISASI

Watoto ambao wameathiriwa na risasi huwa ni wazima tu

Unaweza kujua ikiwa mtoto wako ameathiriwa na risasi akipimwa tu. Watoto wengine huenda:

- Wakaumwa na tumbo, kichwa, wakashindwa kuwa makini, wakakasirika haraka, au wakakosa kula na kulala

MADHARA YA MUDA MREFU

Risasi inaweza kuathiri sehemu zote za mwili na akili



- Kufeli shulenii na kupata alama za chini
- Matatizo ya kusikia na kuongea
- Kukua na kukomaa polepole
- Kukosa utulivu na usumbu
- Kuharibika kwa ubongo, figo na neva

KUMLINDA MTOTO WAKO

Ondoa chanzo cha madini ya risasi na ujihadhari na hatari za madini ya risasi

Watoto huathiriwa na madini ya risasi wakimeza au kupumua madini ya risasi


- Ita wapimaji madini ya risasi kwako (wapime nyumba, udongo na maji)
- Tumia kivuta vumbi cha HEPA na deki za kutupwa kupangusia
- Hakikisha watoto wako mbali na rangi na vumbi ya risasi
- Nawa mikono, vidude vya kuchezza na titibandia mara nyingi
- Epuka vyakula na peremende za nje (peremende za Meksiko)
- Usiwaruhusu watoto wale vidude, funguo, vipambo na mapambo ya vito ya metali—huenda yakawa na madini ya risasi

Toa usaidizi na usisimshaji wa mapema

- Andikisha watoto kwenye mipango ya elimu ya mapema kama vile Head Start, utunzaji wa watoto, chekechea na vikundi vya kuchenza ili iwafanye watamani kujifunza
- Msomee mtoto vitabu na ucheze naye



Ikiwa unaishi kwenye nyumba ya kupanga...



ATHARI YA MADINI YA RISASI KWA WATOTO

Viwango vya Madini ya Risasi katika Damu Vinamaanisha nini kwa Afya ya Mwanao

Madini ya risasi ni hatari na yanaweza kusababisha matatizo ya afya na tabia katika umri wowote. Kipimo cha damu ndiyo njia pekee ya kujua ikiwa mwanao ameathiriwa na madini ya risasi. Watoto wote wanafaa kupimwa wakiwa na umri wa mwaka 1 na 2. Kipimo cha kidoleni ni cha haraka na inaweza kufanyiwa ofisini mwa daktari, na ni tofauti na cha mshipa wa mkononi.

Thibitisha kipimo cha risasi cha damu cha kidoleni na kipimo cha veni cha mkononi.

Kiasi cha Madini ya Risasi kwenye Damu (mikrogramu/desilita)	Cha Mishi pa mido go au ya kawa ida	Wakati wa kupima tena	Je, ninaweza kufanya nini ili nisaidie?
<4	C	Kipimo kingine hakihitajiki ila kama kuna hatari. Pima watoto wa umri wa chini ya miezi 12 baada ya miezi 3-6 kwa kuwa BLL huenda kikaongezeka wakienda hapa na pale.	<ul style="list-style-type: none"> Ongea na daktari wa mtoto wako Lisha mtoto vyakula vyenye Madini ya Kalisi, Chuma na Vitaminini C nyingi Nawa mikono mara kwa mara Safisha kingo za sakafu na vizingiti vya dirisha kwa vitambaa vya kutupwa au deki yenye maji Jihadhari na madini ya risasi ya “Kupelekwa Nyumbani kutoka nje” na vyanzo vingine vya madini ya risasi
	V	Kipimo cha mshipa wakiwa na mwaka 1 na miaka 2. Pima tena kila baada ya miezi 6-12 ikiwa kuna hatari kubwa au hatari imebadilika katika wakati/kipindi fulani.	
4-9	C	Thibitisha baada ya miezi 3-6 ikiwa ana umri wa miaka 3 au chini. Thibitisha kulingana na hatari ikiwa ana miaka zaidi ya 3.. Anaweza kuathirika zaidi katika miezi yenye joto	<p>Endelea kufanya yaliyo hapa juu NA</p> <ul style="list-style-type: none"> Dhibiti hatari za risasi zinazojulikana Endelea kuwapatia lishe nzuri (Madini ya Kalisi, Chuma na Vitaminini C Zingatia kuwapima watoto wengine walioko nyumbani
	V		
10-19	C	Thibitisha ndani ya mwezi 1	<p>Endelea kufanya yaliyo hapa juu NA</p> <ul style="list-style-type: none"> Pima ndugu walio chini ya miaka 6 Hakikisha mtoto anakula ipasavyo/vyakula vinavyofaa Ufuutiliaji wa NH HHLPPP utatoa elimu, kushughulikia kesi/hali, na kutathmini mazingira Zingatia kufanya tathmini ya ukuaji ikiwa viwango vya juu vya risasi kwenye damu vimekithiri
		Pima upya ndani ya miezi 3	